katika mikoa wakilishi (sample) minne (4) ya Dar es Salaam (19/08/2022), Kigoma (22/08/2022), Mwanza (24/08/2022) na Arusha (29/08/2022). Ili kupata maoni ya wadau wanaotumia huduma za usafiri wa reli (TRC), tumepanga kufanya mikutano katika mikoa wakilishi (sample) minne (4) ya Dar es Salaam (19/08/2022), Kigoma (22/08/2022), Mwanza (24/08/2022) na Arusha (29/08/2022). Mikutano hii inaratibiwa kwa kuwashirikisha Wakuu wa Mikoa na Ofisi za LATRA mikoani. Tayari Kigoma na Mwanza mikutano itafanyika katika kumbi za Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Arusha tutawatangazi ukumbi baadae.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Jukumu tunalolifanya hapa leo hii ni kwa mujibu wa Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019 (au Sura ya 413) ambayo inaipa Mamlaka dhamana ya kupitia mapendekezo ya nauli yaliyowasilishwa na mtoa huduma (TRC) kwa kuzingatia uwasilishaji wa taarifa, maoni ya wadau na viashiria muhimu vya uchumi. Mamlaka inajukumu la kuchambua taarifa mbalimbali za kiuchumi kabla ya kutangaza nauli rasmi zitakazo tumika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya maelezo haya, napenda kukufahamisha kuwa Mkutano wetu wa leo utakuwa na sehemu kuu mbili.

1. tutawapa nafasi TRC kuwasilisha mada yao ambapo watapaswa kuonesha uchambuzi uliowawezesha kufikia mapendekezo ya nauli waliyoyatoa, na

